# Global Schools Program




# Muhtasari wa Kozi

## Darasa la 8

**Chanzo:** Reimers, F. (2017). *Empowering students to improve the world in sixty lessons*. Toleo la kwanza. Createspace Independent Publishing Platform.

**Haki ya kunakili:** © 2017 Fernando M. Reimers. Kazi hii imeidhinishwa chini ya leseni ya kimataifa ya Creative Commons Attribution 4.0. Ili kutazama nakala ya leseni hii, tembelea https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/. Haki zote zimehifadhiwa.

**Taarifa:** Maudhui yote yaliyomo humu yameandaliwa na kuchapishwa na Programu ya Shule za Kimataifa (Global Schools Program).

SUSTAINABLE DEVELOPMENT GOALS
17 GOALS TO TRANSFORM OUR WORLD

Global Schools Program

| **Muhtasari** | |
|---|---|
| **Lengo la Kujifunza**<br>Katika darasa la 8, wanafunzi watachunguza maudhui ya ukosefu wa haki: inamaanisha nini, ukosefu wa haki unajidhihirishaje katika maisha ya kila siku, na unachangiaje katika mienendo ya kijamii . Wanafunzi pia, watatathmini maadili yetu, na kujadili umuhimu wa kuhakikisha usawa kwa watu wote, na wachangie njia za kuhamasisha usawa na haki kwenye maisha yao wenyewe. | |
| **Nguzo za Somo** | |
| **Somo 1** | Nini maana ya uonevu/dhuluma kwangu? |
| **Somo 2** | Kwa watu wengine, dhuluma/uonevu ni nini? |
| **Somo 3** | Je, maadili yetu tunayoshirikiana ni yapi na kwanini ni lazima kila mtu achukuliwe kwa usawa? |
| **Somo 4** | Tunaweza kufanya nini? |
| **Somo 5** | Chukua hatua! |
| **Malengo ya kujifunza** | |
| • Wanafunzi wataelewa vyanzo na matokeo ya dhuluma na ukosefu wa usawa duniani.<br>• Wanafunzi wataweza kutambua athari za misukumo ya ukosefu wa haki katika maisha yao wenyewe.<br>• Wanafunzi watawezeshwa kukuza usawa na haki katika maisha yao ya kila siku. | |

**Darasa la 8 Somo 1**

"Ukosefu wa haki ni nini kwangu?"

**Muda:** Dakika: 40
**Masomo:** Maarifa ya Jamii, Uraia, Historia
**Viwango:** Amani, Haki, na Taasisi Imara (MME 16)
**Limebuniwa na:** Maria Lee

**Muhtasari na Mantiki:** Wanafunzi watatakiwa kufikiria kuhusu nyakati ambazo kila mmoja wao alikabiliana na "ukosefu wa haki." Watahimizwa kutafakari kile kilichotokea, kwanini walifikiri hali haikuwa ya haki, na jinsi walivyohisi katika kipindi chote cha hali hiyo. Hatimaye, tungependa wanafunzi waweze kuelewa maana ya ukosefu wa haki, kutambua nyakati ambapo wengine wanakabili ukosefu wa haki, na kutafuta ufumbuzi kama wakala wa haki wa kijamii. Hata hivyo, ili kuweza kuendelea katika hatua hizi, kila mwanafunzi atahitaji kwanza kutambua na kupitia ukosefu wa haki/dhuluma moja kwa moja ili waweze kuwa na wakati rahisi kujihusisha na wengine wanaokabiliwa na dhuluma.

**Lengo la welewa:** Kuwahimiza wanafunzi kutambua na kutafakari nyakati ambazo wao binafsi walipitia ukosefu wa haki (yaani, kujenga ujuzi wa binafsi na uwezo wa kutafakari kwa kina).

**Maswali muhimu:**
- Ukosefu wa haki ni nini kwangu?
- Je, ninafafanuaje/kuelezeaje ukosefu wa haki?
- Je, ninajisikiaje/ninahisije matukio yasiyo ya haki yanaponitokea?
- Je, ukosefu wa haki uliniathirije /unaniathiri vipi

**Malengo ya kujifunza kwa mwanafunzi (Wanafunzi watakuwa na uwezo wa):**
- Kutambua nyakati walizopata hisia fulani.
- Kueleza na kuainisha hisia hizo.
- Kutafsiri hisia hizo kwa maneno.
- Kutafakari kwa nini walipata hisia hizo.

**Upimaji:** Ukaguzi usio rasmi kwa ajili ya kuangalia uelewa.

**Mtiririko wa shughuli:**
- Mwalimu atagawa karatasi ndogondogo kwa kila mwanafunzi na kuwataka waandike ufafanuzi wa "ukosefu wa haki."
- Mwalimu atakusanya karatasi hizo na kuzitia kwenye begi.

- Mwalimu ataendesha mjadala juu ya swali: “Je, umewahi kupitia ukosefu wa haki?”
    - Epuka kutoa mifano yoyote ili  isiathiri majibu ya wanafunzi.
- Wakati wa mjadala, mwalimu atahakikisha kwamba mwanafunzi anayeshiriki agusie: nini kilifanyika, kwanini haikuwa haki, jinsi walivyojiskia, jinsi walivyolichukulia suala hilo.
- Wakati wa kumaliza unapokaribia, mwalimu atachomoa begi lenye karatasi zilizoandikwa ufafanuzi wa ukosefu wa haki hapo awali na kuwapa wanafunzi. Begi litazunguka ili kila mwanafunzi aweze kutoa  karatasi  moja na kusoma kwa sauti ufafanuzi uliomo kwenye karatasi  aliyoitoa kwenye begi.
- Uliza maswali yenye kutaka majibu ya kujieleza kuhusu fasili zinazojitokeza: Una maoni gani kuhusu fasili hizi? Je, unaweza kufafanuaje ukosefu wa haki? Je, ungependa kuongezea chochote?
- Kama darasa, wanafunzi na mwalimu watafikia mwafaka wa  ufafanuzi mmoja madhubuti wa "ukosefu wa haki."

**Nyenzo kwa walimu:**

- https://bokcenter.harvard.edu/leading-discussions
- http://commons.trincoll.edu/ctl/files/2013/08/WEEK-3-10-Strategies-for-Effective-Discussion-Leading.pdf

**Darasa la 8 Somo 2**

"Ukosefu wa haki ni nini kwa Watu Wengine?"

**Muda:** Dakika: 40
**Masomo:** Maarifa ya Jamii, Uraia, Historia
**Viwango:** Uboreshaji Usawa (MME 10); Amani, Haki na Taasisi Imara (MME 16)
**Limebuniwa na:** Maria Lee

**Muhtasari na Mantiki:** Kwa kuwa sasa wanafunzi wameweza kutambua nyakati za ukosefu wa haki katika maisha yao binafsi, itakuwa muhimu kukuza uwezo wao wa kutambua ukosefu wa haki unaotokea kwenye mazingira yanayowazunguka iwe ni katika jamii yao au duniani. Wanafunzi lazima waweze kuona ukosefu wa haki kutoka kwenye mtazamo wa mtu mwingine ili kutambua kwamba wao wenyewe lazima wawe mawakala wa mabadiliko kwa jamii wanapopigania haki kwa niaba ya watu wengine.

**Lengo welewa:** Kuwa na uwezo wa kujiweka katika nafasi ya mtu mwingine kutambua na kukiri matukio ya ukosefu wa haki yanayotokea katika miktadha yao.

**Maswali muhimu:**

- Ukosefu wa haki ni nini?
- Ninatambuaje ukosefu wa haki?
- Watu wengine wanatafsiri au kufafanuaje ukosefu wa haki?
- Ukosefu wa haki unatokea wapi kwa sasa hivi?

**Malengo ya Kujifunza kwa Mwanafunzi (Wanafunzi watakuwa na uwezo wa):**

- Kubainisha matukio ambamo watu hupata ukosefu wa haki.
- Kuchunguza na kutathmini kama kama kuna mtu anapitia hali ya ukosefu wa haki

**Upimaji:** Ukaguzi usio rasmi ili kupima uelewa na majadiliano ya kikundi. Zaidi ya hayo, kwa kuwa sio wanafunzi wote watapata nafasi ya kushirikisha uzoefu wao, wataombwa kuandika kuhusu hilo (huku wakitafakari majadiliano ya kipindi cha leo) kwa mtindo wa uandishi huru kwa kazi ya nyumbani.

**Mtiririko wa shughuli:**

- Kurudia/kuhakiki ufafanuzi wa "haki" kama ambavyo wanafunzi walielezea katika Somo la 1
- Kwa kuzingatia hilo, mwalimu atawapa wanafunzi picha ya kikundi cha watu wanaojiandaa kushiriki kwenye mbio (tazama picha katika sehemu ya nyenzo hapa chini)
- Baada ya wanafunzi kuichunguza picha kwa muda, wanafunzi watagawanywa wawili waili ili waweze kushirikishana mawazo yao. Hakuna maswali maalum yanayoulizwa na mwalimu.
- Darasa linarudi pamoja na mwalimu aongoze majadiliano yanayogusa:
  - Picha hii inahusu nini?
  - Nini kinaendelea kwenye picha hii?
  - Washiriki katika mbio hizo ni nani?
  - Je, mwamuzi anasema nini?
  - Kwanini mwamuzi anasema haya?
  - Ni kwa namna gani anasema/hasemi maneno yaliyosahihi? Je, mbio hizi ni "za haki"?
  - Ni nini kinafanya mbio hizo kuwa sawa?
  - Kwanini ni/sio haki? (Mwalimu acheze kama mtetezi wa shetani)
  - Gusia/ zungumzia:
    - Mitazamo/hali tofauti
    - Jinsi tunavyoweza kutafsiri mambo kwa njia tofauti kutokana na mitazamo tofauti

- Weka majadiliano katika muktadha mkubwa zaidi:
  - Je, kumewahi kutokea matukio ya ukosefu wa haki katika mazingira yetu (ingawa, sio moja kwa moja kwetu)?
  - Je, uliyatambua?
  - Je, watu wengine waliokaribu yako waliyatambua?
  - Je! kuna wakati wengine waliyatambua ila wewe hukuyatambua?
  - Unafikiri tofauti hizi kati ya watu husababishwa na nini?

**Nyenzo kwa walimu:**

- Picha hapo chini:



**Darasa la 8 Somo 3**

“Utu wa binadamu ni nini? Maadili yetu ya pamoja ni yapi? Kwanini usawa kwa kila mtu ni muhimu?

**Muda:** Dakika: 40
**Masomo:** Uraia, Maarifa ya Jamii, Lugha na Mawasiliano
**Viwango:** Amani, Haki na Taasisi Imara (MME 16)
**Limebuniwa na:** Wendi Cui

**Muhtasari na Mantiki:** Katika somo hili, wanafunzi watachunguza dhana za utu wa binadamu, mtanziko wa kijamii, n.k., na kuelewa asili ya matendo ya kibinadamu. Baadaye, watatafakari kile wanachoweza kukifanya kama watazamaji.

**Lengo la welewa:** Wanafunzi watajenga uelewa wa thamani ya pamoja ya ubinadamu.

**Malengo ya Somo:**

- Wanafunzi watajifunza kuhusu sheria za kijamii, utu wa binadamu, mtanziko, shinikizo la kijamii, jukumu la watazamaji, na vitendo vya kibinadamu.

**Maswali muhimu:**

- Utu wa binadamu ni nini?
- Je, tunaweza kufanya nini ili kuulinda utu wa binadamu?
- Kuna hatari gani?

**Malengo ya Kujifunza kwa Mwanafunzi (Wanafunzi watakuwa na uwezo wa):**

- Kuelewa maana ya utu wa mwanadamu
- Kutambua matatizo ya kijamii na kueleza tofauti kati ya majukumu katika mtanziko huo
- Kueleza sababu na hatari za kufanya matendo ya kibinadamu
- Kutafakari  jukumu lao wenyewe katika maisha ya kila siku.

**Upimaji:** Ukaguzi usio rasmi wa kuelewa na kushiriki katika majadiliano ya kikundi.

**Mtiririko wa shughuli:**

- **Ufunguzi (Dakika: 5):**
  - Wanafunzi wanajadiliana katika jozi (wawili wawili) ili kufafanua dhana za "utu na ubinadamu," “mtanziko wa kijamii," na “watazamaji”, kisha kushirikisha darasa lote. Tazama ufafanuzi katika ufunguo
  - "Ufafanuzi" hapa chini.
- **Usomaji wa kidarasa (Dakika: 8):**
  - Walimu wanaweza kutumia “Muuza Duka Jasiri” iliyoorodheshwa katika sehemu ya nyenzo hapa chini, lakini pia wanahimizwa kutafuta hadithi katika muktadha wa kitaifa/ndani.

- **Mjadala katika jozi (Dakika: 10):**
  - Mjadala wa wanafunzi waili juu ya maswali ya mwongozo kutokana na usomaji.

- **Mjadala wa darasa (Dakika: 10):**
  - Mjadala wa kidarasa juu ya maswali ya mwongozo.
  - Uwasilishaji wa mwalimu kwa fasili muhimu.

- **Hitimisho (Dakika: 7):**
  - Tafakari ya mifano mingine halisi ya kimaisha.

**Nyenzo kwa walimu:**

- https://www.usip.org/sites/default/files/GPC_EducatorToolkit-%28HighSchool%29_combined.pdf
- http://cdn.worldslargestlesson.globalgoals.org/2016/06/28_What_is_a_humanitarian_perspective.pdf

**Fasili Muhimu:**

- **Utu /hadhi ya binadamu** unaweza kufafanuliwa kama kujiheshimu
- **Mtazamaji** ni mtu anayefahamu tukio, bila yeye kuhusika, ambapo maisha au hadhi ya binadamu wengine ipo hatarini. Mtazamaji lazima afanye maamuzi ya kuchukua hatua au la, kwani maamuzi yake yanaweza kuyaweka maisha yake au ya yule/wale anaojaribu kusaidia hatarini kimwili au kimali . Chaguo lolote linaweza kuwa na matokeo magumu na ya muda mrefu kwa wote wanaohusika.
- **Shinikizo la kijamii** ni ushawishi unaotolewa na familia, marafiki, au makundi mengine ya watu ambayo huweka shinikizo kwa mtu binafsi kuwa na tabia fulani.

- **Mtanziko** ni hali ya mtu kushindwa kuamua afanye jambo gani miongoni mwa mambo mengine muhimu yanayotakiwa kutekelezwa.
- **Ubinadamu** ni hatua zinazochukuliwa ili kumlinda mtu ambaye maisha yake au utu wake upo hatarini, hasa mtu ambaye kwa kawaida hatungekuwa na ushawishi wa kusaidia kumlinda. Hatua hizo zinaweza kuwa za kumlinda mtu kutokanana na hatari za kimaisha, hatari binafsi au za kimali

**Darasa la 8 Somo 4**

"Tunaweza kufanya nini?"

**Muda:** Dakika: 40
**Masomo:** Maarifa ya Jamii, Sanaa ya Lugha
**Viwango:** Amani, Haki na Taasisi Imara (MME 16)
**Limebuniwa na:** Xin Miao

**Muhtasari na Mantiki:** Katika darasa hili, wanafunzi wanatakiwa kubainisha tukio ambalo walikumbana nalo lenye ukosefu wa haki/walishuhudia ukosefu wa haki kwa watu wengine na kulichambua tukio hilo .

**Malengo ya welewa:**

- Wanafunzi wanatarajiwa kuendeleza muamko wa kutambua tofauti, kuheshimu maadili ya pamoja, kusisitiza mwingiliano wa kibinadamu, na kutafuta mbinu kamilifu za kuongelea ukosefu wa haki. Wanafunzi wataagizwa kutaja mfano wa hali/tukio moja lisilo la haki katika maisha yao binafsi, shuleni, katika jamii au kwenye taarifa za habari.

**Lengo la somo:** Haki ni mada tata ambayo inaweza kuonekana kuwa ya kibinafsi na yenye kutegemea sana mtazamo wa wahusika. Ni ngumu, lakini inakubalika kwenye kushughulikia na kwenye kusuluhisha matukio yenye ukosefu wa haki

**Maswali muhimu:**

- Ukosefu wa haki ni nini kwangu?
- Ukosefu wa haki ni nini kwa wengine?
- Katika ulimwengu wa pamoja tunaoishi, maadili ya pamoja ni yapi?
- Ukosefu wa haki husababishwa na nini??
- Wahusika wakuu kwenye matukio ya ukosefu wa haki ni nani? Ni wajibu wa nani wa kuondoa/kukosoa ukosefu wa haki?
- Je, tafsiri yako/uelewa wako wa ukosefu wa haki unatokana na upande unaounga mkono? kwa vipi?
- Je, unaweza kuchukua hatua pale ukosefu waki unapotokea kwako? Kwa nini utachukua hatua/ kwa nini hautachukua hatua? Kama jibu lako ni ndio, utachukua hatua zipi?

**Malengo ya kuujifunza kwa Mwanafunzi (Wanafunzi watakuwa na uwezo wa):**

- Kushiriki katika kazi ya pamoja, ujuzi wa mawasiliano, na ujuzi wa kuwasilisha.
- Kutumia ujuzi kutoka madarasa matatu (3) yaliyotangulia na uzoefu wa kibinafsi ili kuimarisha dhana ya haki, tofauti, amani, na maadili ya pamoja kama vile huruma na

heshima.
- Kukuza ujuzi wa kuchambua na kutambua pande zinazohusika katika ukosefu wa haki na kujadiliana kwa undani kinachosababisha ukosefu wa haki

**Upimaji:**
- Kujitathmini kwa Mwanafunzi: wanafunzi watatafakari jinsi walivyoshirikiana vyema na wenzao na jinsi walivyowasilisha mawazo yao darasani .
- Tathmini ya Mwalimu: mwitiko ulioandikwa pamoja na maoni ya kujitathmini kwa wanafunzi.

**Mtiririko wa shughuli:**
- **Chemsha bongo:** Waalike wanafunzi kushirikisha baadhi ya matukio ya ukosefu wa haki waliyokutana nayo.
- **Shughuli:** Wasilisha picha au video za ukosefu wa haki katika hali tofauti (k.m. kesi mahususi za mahakama ambazo ni za eneo na nchi mahususi).
- **Kuunda Makundi:** Tambua na uchambue hali moja isiyo ya haki. Elezea ni kwa namna ipi haki ingetendeka
- **Uwasilishaji wa kikundi:**
    - Wanafunzi wawasilishe darasani jinsi walivyokosoa ukosefu wa haki katika vikundi vyao. Kama darasa, wanafunzi wanajadili suluhu zilizopendekezwa na vikundi, wakizingatia ufafanuzi wa haki na mtazamo
    - Wanafunzi wanajaribu kujibu maswali yafuatayo:
        - Je, mtazamo una umuhimu?
        - Mtazamo wa nani ni muhimu?
        - Kwa nini mtazamo ni muhimu na unahusiana vipi na haki, (ikiwa ni wa muhimu)?

**Nyenzo kwa walimu:**
- *Justice* by Michael J. Sandel
- https://www.youtube.com/watch?v=-3cDFEw1bhY
- https://www.youtube.com/watch?v=AjwL5vWqp-Y
- https://www.youtube.com/watch?v=OxbfjxyPEPk

**Darasa la 8 Somo 5**

“Kutafuta Suluhu kwa Ubunifu Kushughulikia Hali Isiyo ya haki”

**Muda:** Dakika: 60
**Masomo:** Maarifa ya Jamii, Sanaa ya Lugha
**Viwango:** Amani, Haki na Taasisi Imara (MME 16)
**Limebuniwa na:** Xin Miao

**Muhtasari na Mantiki:** Katika darasa hili, wanafunzi wanatarajiwa kuendeleza somo lililopita na kujitahidi kuorodhesha changamoto walizokutana nazo wakati wa kupendekeza suluhu. Kama darasa, wanafunzi watachagua tukio moja la ukosefu wa haki ambalo watalijadili na kuandaa mpango wa kina wa kuondoa ukosefu wa haki uliopo kwenye tukio hilo.

**Malengo ya welewa:**

- Wanafunzi watafute suluhisho la hali waliyokubaliana nayo kuwa ina ukosefu wa haki
- Wanafunzi wajifunze jinsi ya kuandaa mipango ya utekelezaji kuondoa ukosefu wa haki

**Malengo ya Somo:**

- Wanafunzi wataelewa kuwa wanao uwezo wa kuleta mabadiliko katika matukio ya hali halisi ya kila siku ya ukosefu wa haki kwa kufanya kazi kwa ushirikiano na kufuatilia mifano ya mawakala wa mabadiliko wanaoongelea masuala ya ukosefu wa haki.

**Maswali Muhimu:**

- Je, ni watu gani hushughulikia ukosefu wa haki?
- Watu hushughulikiaje ukosefu wa haki?
- Je, mtu binafsi anaweza kufanya nini kushughulikia ukosefu wa haki?
- Je, kila mtu katika jamii hukubaliana kila mara ni mambo gani ni ya haki na ni yapi yasiyo ya haki?
- Wakati wa kushughulikia suala lisilo la haki ni hatua gani kama kundi linapaswa kuchukua?
- Je, taasisi mbalimbali zingefanya nini ili ziweze kushughulikia ukosefu wa haki, kama vile kwenye mitandao ya kijamii, vyombo vya sheria, serikali, n.k ?
- Kuna tofauti gani kati ya jitihada zinazofanywa na mamlaka za ngazi za chini na zile za kisiasa?

**Malengo ya Kujifunza kwa Mwanafunzi (Wanafunzi watakuwa na uwezo wa):**

- Kujenga ustadi wa kuchambua, mazungumzo, mawasiliano, na ujuzi wa kuwasilisha
- Kutafiti na kuchambua harakati za haki za kijamii

- Kuunganisha utafiti na kutengeneza  mkakati

**Upimaji:**

- Wanafunzi waandike tafakari ya jinsi wanavyoelewa ukosefu wa haki, na namna wanavyoamini hii inalinganishwa na jinsi walivyowasilisha mawazo yao wakati wa darasa.
- Tathmini ya mwalimu ni fungu la maoni na mwitiko kwa tafakari za wanafunzi.

**Mtiririko wa Shughuli:**

- Hatua ya 1 (Dakika: 10): Mwalimu anatanguliza harakati kadhaa za haki za kijamii ambazo ni mahususi kwa muktadha au zinazotambulika kimataifa na kuwataka wanafunzi kutafuta mfanano/tofauti katika harakati hizo.

- Hatua ya 2 (Dakika: 5): Wanafunzi wanaombwa kutafakari juu ya darasa lililopita na mada walizowasilisha katika vikundi vidogo. Kisha wanafunzi wanapiga kura juu ya mada ya kujadiliwa darasani.

- Hatua ya 3 (Dakika: 25): Wanafunzi wanajadili mada ya dhuluma/Ukosefu wa haki na wajadili suluhisho linalowezekana. Wanafunzi wanafikiri kuhusu wadau ambao dhuluma/ukosefu wa haki unawaathiri na kuchora mitazamo ya wadau kwenye ubao (jinsi makundi mbalimbali yanavyohisi kuhusu hilo).

- Hatua ya 4 (Dakika: 15): Wanafunzi wanajadiliana kuhusu suluhu ambayo itashughulikia maslahi ya wadau wengi. Wanafunzi hupanga na kuwasilisha suluhisho lao.

- Hatua ya 5 (Dakika: 5): Hotuba/ Maneno ya kufunga na tafakari.